**Gazeti Makhsus**

# *GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR*

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXIV Nam. 7355** **12 Juni, 2025** **Bei Shs. 5,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Kodi na Tozo na Kurekebisha Baadhi ya Sheria Zinazohusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Umma na mambo mengine yanayohusiana na hayo ......................................... 875

**SEHEMU YA SHERIA**

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Mswada**

Nam: Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi

---

**T A N G A Z O**

**ZANZIBAR**
12 Juni, 2025

(Mhandisi. Zena Ahmed Said)
***Katibu wa Baraza la Mapinduzi na***
***Katibu Mkuu Kiongozi***.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**

*wa*

**SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUBADILISHA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2025 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI NA UTARATIBU WA KODI, NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 18.

**4.** Kifungu cha 18 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (4) kama ifuatavyo:

"(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Kamishna Mkuu anaweza, baada ya kushauriana na Waziri, kuongeza tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ritani ya kodi ama kwa ujumla, kwa sekta au kundi la walipa kodi endapo kuna sababu ya msingi ya kuongezwa huko."

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**5.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuogeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Mtu yeyote anayeendesha mfumo wa kielektroniki ataunganisha mfumo huo na mfumo wa Mamlaka kwa madhumuni ya kodi."

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (2), (3), (4), (5), (6) na

(7) kuwa vifungu vidogo vya (3), (4), (5), (6), (7) na (8).

(c) kuogeza kifungu kidogo kipya cha (9) mara baada ya kifungu kidogo cha (8) kama ifuatavyo:

"(9) Mtu yeyote atakayeshindwa kuunganisha mfumo wake na mfumo wa Mamlaka kwa mujibu wa kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au kifungo kisichopungua kipindi cha miaka miwili."

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**6.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**7.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta ufafanuzi wa neno "mkaazi" na kuweka badala yake ufafanuzi mpya kama ifuatavyo:

"mkaazi" maana yake ni mtu binafsi, kampuni, taasisi ya amana, jumuiya, ubia, taasisi ya serikali, au taasisi nyengine ya kisheria ambayo makaazi yake au uanzilishi wake upo Zanzibar.

Marekebisho ya kifungu cha 4A.

**8.** Kifungu cha 4A cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Endapo haitowezekana kuteua mwakilishi wa kodi kutokana na mazingira yake ya kibiashara, mtu ambaye siyo mkaazi ataomba kwa Kamishna Mkuu kusajiliwa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika Kanuni za Usimamizi na Utaratibu wa Kodi (Utaratibu wa Usajili uliorahisishwa kwa Watoa Huduma za Kielektroniki kwa Wasio Wakaazi na Watoa Huduma za Kitalii wa Kigeni), 2022".

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**9.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) cha kifungu hiki, utoaji wa huduma hautatozwa kodi ya sifuri ikiwa:

(a) utoaji huo ni wa haki au chaguo la kupokea huduma nyengine Zanzibar; au

(b) huduma zimetolewa chini ya makubaliano na asiye mkaazi lakini zinatolewa kwa mtu aliyopo Zanzibar ambaye hajasajiliwa.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA BIDHAA, NAM. 8 YA 2017

Kusomwa.

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marakebisho ya kifungu cha 3.

**11.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (f) katika ufafanuzi wa maneno "thamani inayotozwa ushuru" kama ifuatavyo:

"(f) huduma nyengine inayoingizwa isipokuwa huduma za kifedha, kiwango, tozo au jumla ya thamani ya huduma inayopatikana kutoka kwa watoaji huduma wa kigeni."

Marekebisho ya kifungu cha 15.

**12.** Kifungu cha 15 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) msamaha wa ulipaji ushuru chini ya kifungu hiki hautotumika kwa vyombo vya moto kuanzia miaka mitano."

(b) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa (4).

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA HOTELI, NAM. 1 YA 1995

Kusomwa.

**13.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Hoteli, Nam. 1 ya 1995 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**14.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Kutakuwa na punguzo la kiwango katika ushuru wa hoteli kulingana na kiwango cha ushuru kinachostahiki kulipwa na mtu kutoka nje ya Zanzibar."

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (3) na (4) kuwa vifungu vidogo vya (4) na (5).

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR, NAM. 5 YA 2006

Kusomwa.

**15.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usafiri Baharini Zanzibar, Nam.5 ya 2006 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 13A.

**16.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A mara baada ya kifungu cha 13 kama ifuatavyo:

"Uwasilishaji wa Cheti cha Kuthibitisha Ulipaji wa Ushuru wa Forodha.

**13A.** Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13 cha Sheria hii, mmiliki au wakala wa chombo cha baharini kinachokusudiwa kusajiliwa Zanzibar atawasilisha Cheti cha Kuthibitisha Ulipaji wa Ushuru wa Forodha kilichotolewa na mamlaka ya forodha husika."

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR, NAM. 11 YA 2022

Kusomwa.

**17.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Nam.11 ya 2022 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Kuongeza kifungu kipya cha 18A.

**18.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo:

"Uteuzi wa Naibu Kamishna Mkuu.

**18A.-**(1) Kutakuwa na Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Naibu Kamishna Mkuu ikiwa mtu huyo ana sifa sawa za kuteuliwa kama Kamishna Mkuu.

(3) Naibu Kamishna Mkuu atakuwa Msaidizi Mkuu wa Kamishna Mkuu kwa ajili ya kutekeleza kazi za kila siku za Mamlaka".

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA VYOMBO VYA MOTO (KUMLINDA MTU WA TATU), SURA YA 136 YA 1953

Kusomwa.

**19.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Vyombo vya Moto (Kumlinda Mtu wa Tatu), Sura ya 136 ya 1953 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**20.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "isiyozidi Shilingi Elfu Mbili" aliyojitokeza katika kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake maneno " isiyozidi Shilingi Laki Moja."

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni ya Mswada huu ni kuweka na kurekebisha baadhi ya kodi na ushuru, na kufanya marekebisho ya sheria za fedha na kodi zinazohusiana na ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hizo.

Kodi na ushuru uliowekwa zinakusudiwa kukusanywa na mamlaka za kodi na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kama mapato ya Serikali. Marekebisho ya sheria za kodi yanakusudia kurahisisha taratibu za ukusanyaji wa kodi, kuzifanya sheria za kodi ziendane na wakati kwa mujibu wa hali ya sasa na kuongeza mapato ya Serikali bila ya kuathiri maslahi ya umma.

Mswada huu umegawanyika katika Sehemu Nane:

***Sehemu ya Kwanza*****:** inajumuisha jina fupi na kuanza kutumika Pamoja na marekebisho ya sheria mbalimbali.

***Sehemu ya Pili*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 katika kifungu cha 18 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (4) na 23 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2).

***Sehemu ya Tatu*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998 katika kifungu cha 2 kwa kufuta ufafanuzi wa neno mkaazi na kuweka badala yake ufafanuzi mpya wa neno kwa ajili ya kuongeza wigo wa ufafanuzi wa neno mkaazi, 4A kwa kuongeza kifungu kidogo cha (5) na 9 kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3).

***Sehemu ya Nne*****:** inapedekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Nam. 8 ya 2017 katika kifungu cha 3 kwa kuongeza aya mpya ya (f) na 15 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (3) pamoja kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha (4).

***Sehemu ya Tano*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli, Nam. 1 ya 1995 katika kifungu cha 3 kwa kuongeza kifungu kipya cha (3) mara baada ya kifungu cha (2) na kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (3) na (4) kuwa (4) na (5) .

***Sehemu ya Sita*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Usafiri Baharini Zanzibar, Nam. 5 ya 2006 kwa kuongeza kifungu kipya cha 13A ambacho kinahusiana na uwasilishaji wa Cheti cha kuthibitisha ulipaji wa Ushuru wa Forodha.

***Sehemu ya Saba*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Nam. 11 ya 2022 kwa kuongeza kifungu cha 18A ambacho kinahusiana na uteuzi wa Naibu Kamishna Mkuu.

***Sehemu ya Nane*****:** inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Vyombo vya Moto (Kumlinda Mtu wa Tatu), Sura ya 136 ya 1953 katika kifungu cha 3.

**ZANZIBAR** **(DKT. SAADA MKUYA SALUM)**
12 Juni, 2025 **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS,**
**FEDHA NA MIPANGO**

**LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR-2025**